**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI WA MTIHANI WA KABLA YA**

**MTIHANI WA TAIFA (PRE – NECTA)**

**MKOA WA IRINGA**

**KISWAHILI 2**

1 ." Fasihi simulizi huchomoza katika jamii ambayo inaandamwa na mabadiliko ya namna mbalimbali”. Thibitisha dai hili kwa kutumia hoja tano (5) ukionesha mabadiliko ya uhifadhi wa fasihi simulizi.

Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha mabadiliko ya uhifadhi wa fasihi simulizi kwa kutumia njia zifuatazo.

-Kanda za kunasia sauti

-Video

-Filamu za sinema .

-Redio .

-Runinga/Televisheni .

*Afafanue hoja hizo kwa mifano halisi.*

*Hoja 5@ 02 jumla alama 10.*

2 . "Si kila mwenye ulimi anaweza akawa msimulizi mzuri”. Fafanua kauli hii kwa kutoa hoja tano (5).

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza sifa za msimulizi.

-Msimulizi lazima awe na uwezo wa kuiunda upya simulizi yake kila anapoiwasilisha.

-Msimulizi lazima ajue vyema utamaduni wa jamii yake.

-Msimulizi huwa ni bingwa wa lugha yake.

-Msimulizi lazima awe na tabia ya kuvutia pamoja na kipawa cha kufurahisha watu.

-Msimulizi lazima awe hodari wa kuifahamu tabia za binadamu.

-Msimulizi anapaswa kuwa na ujuzi wa kuifahamu hadhira yake pamoja na matarajio ya hadhira yake.

*Mtahiniwa afafanue kwa mifano halisi.*

*Hoja 5 @ 02 jumla alama 10*

3 . Je kuna fasihi ya Kiswahili? Toa msimamo wako kwa mifano dhahiri. Toa hoja tano (5).

Mtahiniwa athibitishe kuwa kuna fasihi ya Kiswahili kwa kutumia hoja madhubuti zenye mifano.

Hoja

-Kuna fasihi zinazoelezea  mazingira ya mswahili.

Mfano: "Nyota ya Rehema"(anazungumzia kukataa watoto).

-Mila na desturi za waswahili.

Mfano: Kuchaguliwa mchumba.

-Methali, Nahau,Misemo inasheheni mazingira ya mswahili.

Mfano:" Kusadikika” (msema kweli hukimbiwa na  wenzake).

-Hadidhi mbalimbali za Kiswahili.

Mfano: masimulizi ya Alfa lela Ulela na Hekaya za Abunuasi.

-Kuzungumzia maisha halisi ya mswahili.

Mfano: matumizi ya vitu vy asili.

*Hoja zenye mfano 5@ 02*

*jumla alma 10*

4 . Soma matini ifuatayo, kisha bainisha vipengele kumi vya matumizi ya lugha.

Mtahiniwa abainishe vipengele kumi vya matumizi ya lugha.

-Kutohoa maneno

mfano: taksi.

-Mdokezo

mfano: hivyo?..........

-Nidaa

mfano: Naam!, si haki!

-Matumizi ya lugha ya kingereza

mfano: "house for sale”

-Tashtiti

mfano: unauza nyumba hii?

-Tashihisi

mfano: Lakini wewe ni mtoto.

-Msemo

mfano: mimi mwana wa haramu.

-Tashbiha

mfano: mimi mwana wa haramu kama hujui.

-Mchezo wa maneno

mfano: Ndo utajua hujui.

-Tafsida

mfano: wakati walipomzika Martha alikuwa hayupo duniani.

-Methali

mfano: mbuzi wa maskini hazai.

*Kila kipengele chenye mfano @ 01*

*Jumla alama 10*

5. Waandishi anuai wametumia vizuri wakati uchwao ili kuibeba jamii na kuifikisha sehemu mahususi kwa kutumia wahusika mbalimbali, Eleza jinsi gani wahusika wawili uliosoma kazi zao walivyofanya juhudi ya kujenga maisha mapya na endelevu kwa mifano dhahiri.Toa hoja nne (4) kwa kila kitabu.

Mtahiniwa atoe utangulizi unaofafanua Zaidi kiini cha swali. Swali lilimtaka aeleze jinsi gani wahusika walivyofanya juhudi katika kujenga maisha mapya na endelevu kwa mifano dhahiri.

FUNGATE YA UHURU

-Umuhimu wa uongozi bora

-Umoja na mshikamano ni njia mojawapo ya ujenzi wa jamii mpya.

-Ujasiri, kujitoa mhanga na uzalendo ni njia mojawapo ya ujenzi wa jamii mpya.

-Ukoloni mamboleo ni kikwazo cha ujenzi wa jamii mpya.

-Mapenzi ya kweli ni yale yasiyojali fedha au hali ya mtu.

CHUNGU TAMU

-Ni lazima tujitoe mhanga ili kutetea wanyonge.

-Dhuluma, unyonyaji, uzembe ni vikwazo vya ujenzi wa jamii mpya.

-Demokrasia ya kweli ndiyo njia pekee ya ujenzi wa jamii mpya.

-Umuhimu wa uongozi bora.

-Matabaka husababisha kukosekana kwa umoja na mshikamano.

KIMBUNGA

-Mapenzi na ndoa ya dhati ni muhimu katika jamii zetu.

-Maadili mema na maono ni pekee ya kuiweka jamii katika misingi ya haki.

-Uongozi mzuri.

-Ukoloni mamboleo, rushwa ni miongoni mwa vikwazo vya ujenzi

-Umuhimu wa malezi bora.

MAPENZI BORA

-Umuhimu wa mapenzi bora.

-Hasara za kukosekana kwa mapenzi bora.

-Faida za mapenzi bora.

Mtahiniwa atoe hitimisho safi.

*Utangulizi alama 02*

*Kiini hoja 4 zenye mifano kwa kila kitabu @02*

*Hitimisho 02*

*Jumla alama 20.*

6 . Mwanafasihi ni mtu muhimu sana katika jamii kwani kazi yake kuu ni kuelimisha jamii nzima inayomzunguka kwa kutumia fasihi. Nini tofauti kuu ya fasihi na matawi mengine ya Sanaa? Eleza tofauti hii kwa kuonesha jinsi wasanii walivyoitumia katika vitabu viwili ulivyosoma kwa kutoa hoja nne (4) kwa kila kitabu

Mtahiniwa atoe utangulizi unaoeleza maana ya fasihi na Sanaa na afafanue swali kuwa tofauti kuu ya fasihi na matawi mengine ya sanaa ni fasihi kutumia lugha.

Mtahiniwa aeleze matumizi ya lugha kama ifuatavyo;

MAPENZI BORA

-Tashbiha

.Mapenzi ya kuhimili ya ladha kama asali.

.Chozi litatirirka mfano kama gharika.

-Sitiari

.Mapenzi kwetu dhahabu tuwe nayo kiarabu.

.Dunia tunayokaa jangwa tupu la ukiwa.

-Mbaalagha

.Nyuso zote zinatota kwa bahari ya machozi.

.Nyuso zikifanya mito ya machozi ya fukuto.

-Tashihisi

.Tunachekwa na wadudu wajinga wa kuabudu.

-Takriri

.Choyo

.Chuki

CHUNGU TAMU

-Msemo

.Sasa mwaleta shari.

.Kuvaa masulupwete.

-Methali

Umoja ni nguvu.

-Tashbiha

.Maoni yetu chakavu sawa na nguo ya miaka.

.Shaba kama maji.

-Tashihisi

.Kifo kimeniita

.Kicheche pia ameapa.

-Sitiari

.Ushairi ni sukari tamu.

.Umaskini ni mzigo.

-Tafsida

.Usiwe mwonja asali

.Dora ana kitu tumboni.

-Kejeli

.Jina lenye ugonjwa wa kaka.

.Iweje binti shibe aende kwa ombaomba.

FUNGATE YA UHURU

-Misemo

.Waja wa Mungu

.Utakiona cha mtema kuni.

-Tashbiha

.Kitandani nilalapo kama dema la samaki

.Mbu ndani kama ndege wa vitani.

-Sitiari

.Bao la mkahawani kila mtu akaliya

.Sasa jamvi la wageni wajapo huwapokea

-Kejeli

.Fungate – viongozi wanaofaidi Fungate

.Kuntu sauti ya kiza –Nyuki kukejeli baadhi ya tabia chafu.

-Tafsida

.Paka shume – Tabia ya kumendea vitu.

KIMBUNGA

-Tashbiha

.Ufedhuri na uovu kama yake mazoeya

.Awe kama malaika mzuri kupindukiya.

-Tafsida

.Paka – wizi

-Taswira

.Kimbunga - Kuashiria mapinduzi

.Nyani - kuashiria wananchi waliosalitiwa.

-Takriri

.Kujitawala – msisitizo.

Mtahiniwa atoe hitimisho safi linaloendana na swali.

*Utangulizi alama 02*

*Hoja zenye mifano 4 kwa kila kitabu @ 02*

*Hitimisho zuri alama 02*

*Jumla alama 20*

7 . Riwaya za waandishi wetu hutuletea ujumbe mpya lakini wakati mwingine hutuletea ujumbe uliopitwa na wakati, chagua riwaya mbili ulizosoma na onesha jinsi ujumbe wake ulivyopitwa na wakati. Tumia hoja nne (4) kwa kila kitabu.

Mtahiniwa atoe utangulizi unaokidhi matakwa ya swali.

Kwenye kiini cha swali aoneshe ujumbe uliopitwa na wakati.

USIKU UTAKAPOKWISHA

-Mwanamke kuwa chombo muhimu cha kujipatia fedha

Mfano: Gonza kumshawishi Chioko aongee na mpenzi wake Nelli ajiuze ili wapate fedha.

-Kufuata mila na matakwa ya mila potofu

Mfano: Chioko kulinda makaburi.

-Kuiba ni suluhisho la kuondokana na umaskini

Mfano: Gonza na Nyundo

-Kutoa rushwa ni chanzo cha kupata ajira

Mfano: Gonza kuambiwa atoe rushwa ilia pate ajira.

VUTA N’ KUVUTE

-Kukubali kuwekwa utawani kwa mwanamke

Mfano: Shihab kumweka Yasmini utawani.

-Kukubali kuchaguliwa mchumba na wazazi

Mfano: Yasmini kuchaguliwa mume na wazazi.

-Kumwozesha binti mdogo kwa mtu mzima

Mfano: Mara tu baada ya kuvunja ungo Yasmini aliozeshwa mume.

-Kumpenda mtu kwa sababu ya pesa

Mfano: Mwajuma kumlazimisha Yasmini aolewe na Shihabu kwa sababu ya pesa.

MFADHILI

-Kukubali kurudiana na mume ili watoto wawe na baba mmoja.

Mfano: Dania alikubali kurudiana na Jerry ili walee watoto pamoja.

-Ulevi wa kupindukia ili kusahau matatizo

Mfano: Gaddibullahalianza kunywa sana pombe ili asahau matatizo.

-Kutoa ufadhili kwa siri siyo suluhisho la matatizo.

Mfano: Gaddibullah alimwambia Docta Villan asimwambie Dania kuwa yeye ndiye aliyetoa Ini.

-Mapenzi ni suluhisho la matatizo yote duniani

Mfano: Gaddibullah kuanzisha mapenzi na Dania baada ya kusalitiwa na mke wake Nyambuja.

KUFIKIRIKA

-Suluhisho la matatizo ni kwenda kwa waganga wa kienyeji

Mfano: mfalme kuwaita waganga wote ili kutafuta suluhisho la tatizo la ugumba na utasa.

-Kumfundisha mwanafunzi mambo mengi sana muda wote siyo suluhisho la mafanikio.

Mfano: Mtoto wa mfalme alifundishwa muda wote bila kupewa muda wa kupumzika hali iliyomsababishia kuugua.

-Ujinga au werevu wa mtu hauangaliwi kutokana na kazi anayofanya mtu

Mfano: Mwerevu alipokamatwa alitetemeka na hakujua jinsi ya kujiokoa.

-Haiwezekani nchi yote kugeuka jangwa kutokana na uchimbaji wa dawa ya mfalme.

Mfano: Waganga wa mitishamba walikata miti yote nchi ikageuka jangwa.

Mtahiniwa atoe hitimisho safi kulingana na swali.

*Utangulizi alama 02*

*Hoja 4 kila kitabu @ 02*

*Hitimisho alama 02*

*Jumla alama 20*

8 . Mara nyingi msanii wa kazi yoyote ya kifasihi anapoandika kazi yake huwa anazingatia uwiano baina ya fani na maudhui ili jamii anayoiandikia ijifunze. Lakini ili awe tofauti na mwingine huzingatia Zaidi mtindo. Jadili mtindo uliotumika katika tamthiliya mbili ulizosoma kama mbinu ya kifani. Toa hoja nne (4) kwa kila kitabu.

Mtahiniwa atoe utangulizi unaoeleza maana ya mtindo katika fasihi. Utangulizi wake pia lazima uhusishe vitabu atakavyotumia.

MORANI

-Dialojia (majibizano).

-Maelezo ya majibizano.

-Matumizi ya nafsi zote tatu.

-Matumizi ya nyimbo (uk.43)

NGUZO MAMA

-Daiolojia(majibizano).

-Masimulizi.

-Lugha ya kishairi.

-Matumizi ya nyimbo.

-Mianzo ya hadidhi ya fasihi simulizi.

-Matumizi ya nafsi zote tatu.

KWENYE UKINGO WA THIM.

-Daiolojia (majibizano)

-Matumizi ya nafsi zote tatu.

-Masimulizi.

KIVULI KINAISHI

-Changamano

-Monolojia (masimulizi)

-Matumizi ya nafsi zote tatu.

-Matumizi ya tanzu zote tatu

Mfano: Ngano, Ushairi na Tamthiliya.

Mtahiniwa atoe hitimisho safi linaloendana na swali.

*Utangulizi alama 02*

*Hoja 4 kila kitabu @ 02*

*Hitimisho alama 02*

*Jumla alama 20*